

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



BUNGE LA TANZANIA

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA
UTALII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ARDHI,
NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MWAKA WA FEDHA
2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO
YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA
WA FEDHA 2026/2027**

*[Inatolewa Chini ya Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge
za mwaka, 2025]*

Ofisi ya Bunge,
Idara ya Kamati za Bunge,
DODOMA.

YALIYOMO

Ukurasa

YALIYOMO	i
ORODHA YA VIELELEZO	ii
SEHEMU YA KWANZA	1
1.0 MAELEZO YA JUMLA	1
1.1 Utangulizi.....	1
1.2 Muundo wa Taarifa	1
1.3 Msingi wa Uchambuzi.....	2
1.4 Mawanda ya Uchambuzi wa Taarifa	3
SEHEMU YA PILI	5
2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI	5
2.1 Ufafanuzi wa Jumla.....	5
2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.....	5
2.2.1 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati	6
2.2.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026	7
2.2.2.1 Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.....	8
2.2.2.2 Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03)	12
2.2.2.3 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi	12
2.2.3 Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026	14
2.2.4 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kutoka Hazina.....	15
2.3 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027.....	18
2.3.1 Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027	19
2.3.2 Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027	21
2.3.3 Mambo Mahsusi Yanayogusa Sekta ya Ardhi.....	23
SEHEMU YA TATU	31
3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI	31
3.1 Maoni ya Jumla	31
3.2 Ushauri wa Kamati katika Maeneo Mahsusi kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.....	31
3.3 HITIMISHO	36

ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na.: 1	Ukusanyaji wa Maduhuli kufikia Mei, 2026.....	14
Kielelezo Na. 2:	Upatikanaji wa Fedha kwa Fungu 48	16
Kielelezo Na. 3:	Upatikanaji wa Fedha (Fungu 03)	17
Kielelezo Na. 4:	Ulinganisho wa Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027 Fungu 48	19
Kielelezo Na. 5:	U linganisho wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2025/2026 na 2026/2027	20
Kielelezo Na. 6:	Ulinganisho wa Bajeti ya Fungu 48 kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026 na 2026/2027	22
Kielelezo Na. 7:	Ulinganisho wa Bajeti ya Fungu 03 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027	23

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA
UTALII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ARDHI,
NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MWAKA WA FEDHA
2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO
YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA
MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAELEZO YA JUMLA

1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

1.2 Muundo wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, Muundo wa Taarifa hii unatokana na masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Kudumu za Bunge ya mwaka 2025 inayozungumzia Muundo wa Taarifa inayowasilishwa Bungeni. Taarifa hii imegawanyika katika sehemu tatu zifuatazo: -

- (i) Sehemu ya kwanza ni utangulizi inayotoa Msingi wa Uchambuzi na Mawanda ya Uchambuzi;
- (ii) Sehemu ya pili inayochambua na kufanya tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027; na
- (iii) Sehemu ya tatu inayofafanua Maoni ya Kamati na ushauri unaotolewa kwa Serikali pamoja na kuhitimisha Taarifa ya Uchambuzi wa Bajeti.

1.3 Msingi wa Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, Msingi wa Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Ardhi unatokana na Masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka, 2025. Kanuni ya 121 (4) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 7(1)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inahusu uchambuzi huo.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi masharti hayo, Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (**Fungu 48**) pamoja na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (**Fungu 03**) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka

wa Fedha 2026/2027. Taarifa hii inatokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati wakati inachambua Bajeti ya Wizara hii.

1.4 Mawanda ya Uchambuzi wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inahusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (**Fungu 48**) pamoja na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (**Fungu 03**) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi iliyochambuliwa inahusu maeneo yafuatayo: -

- (i) Mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (**Fungu 48**) na Bajeti ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (**Fungu 03**) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;
- (ii) Utekelezaji wa kazi zilizofanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (**Fungu 48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (**Fungu 03**) kufikia mwezi Februari, 2026;
- (iii) Uzingatiaji wa Ushauri na Maoni ya Kamati uliotolewa Bungeni wakati wa kupitisha Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (**Fungu 48**) na Bajeti ya

Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (**Fungu 03**)
kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

- (iv) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha
2026/2027.

SEHEMU YA PILI

2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

2.1 Ufafanuzi wa Jumla

Mheshimiwa Spika, sehemu hii ya Taarifa inaelezea msingi wa ushauri wa Kamati uliotokana na Hoja ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kanuni ya 120 (1) na (2) inazitaka Kamati za Kisekta kufanya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha unaoisha na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata.

2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, mara baada ya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03). Masuala yaliyochambuliwa ni pamoja na: -

- (i) Utekelezaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;
- (ii) Hali ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;
- (iii) Hali ya ukusanyaji wa maduhuli; na

(iv) Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.

2.2.1 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, katika kulisaidia Bunge kutekeleza jukumu lake la kuishauri Serikali, tarehe 29 Mei, 2025, wakati wa uwasilishwaji wa Hotuba ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa Maoni na Ushauri kuhusu mambo saba (7). Ili kupima tija ya Bunge kuendelea kuishauri Serikali, Kamati ilitaka kubaini iwapo ushauri uliotolewa umezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 23 Machi, 2026, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi alifika mbele ya Kamati kuwasilisha taarifa kuhusu hatua iliyofikiwa katika kutekeleza ushauri wa Kamati.

Kamati ilichambua taarifa na kubaini kwamba, mambo manne yamezingatiwa na utekelezaji wake upo katika hatua mbalimbali. Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua hiyo na kuendelea kuisitiza kuzingatia maoni na ushauri unaotolewa na Kamati na Waheshimiwa Wabunge katika kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa Maoni matatu yafuatayo:-

- (i) Katika Programu ya KKK, Kamati ilishauri Serikali kuongeza kasi ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha kufikia **viwanja 100,000** ifikapo Juni, 2026. Taarifa ya Utekelezaji ilionyesha kuwa, upimaji umefikia viwanja 24,326 sawa na asilimia 24 ya lengo. Kamati haikuridhishwa na kasi hii kwani haioneshi uwezekano wa kufikia lengo la viwanja 100,000 ifikapo Juni, 2026. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa lengo linafikiwa ili kuongeza mapato;
- (ii) Serikali kushindwa kuonesha hatua za kisheria zilizochukuliwa kwa wawekezaji 31 waliobainika kutozingatia masharti ya umiliki wa ardhi; na
- (iii) Serikali kushindwa kuirejeshea Wizara ya Ardhi **asilimia 20** ya makusanyo yanayotokana na kodi ya pango la ardhi (*land rent*).

2.2.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika mikoa miwili (2) ya Kilimanjaro na Tanga ili kukagua Miradi minne (4) inayotekelezwa na Wizara kama ifuatavyo:-

2.2.2.1 Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

(a) Mradi Na. 2324: Uimarishaji Mipaka ya Kimataifa - kipande cha IV na V Tarakea - Rombo hadi Mkomazi - Mwanga

Mheshimiwa Spika, Mwaka wa Fedha 2025/2026 Mradi huu ulitengewa **Shilingi 1,000,000,000**. Hadi Kamati inakagua Mradi huu ulikuwa umepokea **Shilingi 900,000,000** sawa na asilimia 90.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifahamishwa kuwa kufikia Machi, 2026 mpaka ulikuwa umeimarishwa kwa umbali wa Kilomita 564 kati ya Kilomita 758, sawa na asilimia 75. Kamati iliridhishwa na hatua ya utekelezaji na kuishauri Serikali kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha kazi ya uimarishaji wa mipaka. Aidha, Kamati inahimiza ushirikishwaji wa wananchi katika zoezi hili ili kuepuka migogoro itokanayo na wananchi kutoelewa dhana ya uimarishaji wa mipaka.

(b) Mradi Na. 2326: Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK) katika Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe

Mheshimiwa Spika, Mradi huu ni Programu ya miaka 10 unaotekelezwa na Wizara ya Ardhi, kwa kushirikiana na Halmashauri mbalimbali Nchini unaotarajiwa kukamilika mwaka 2028/2029.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Programu hii ilitoa **Shilingi 180,000,000** kwa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ambazo zimetumika kuchora michoro 5 ya mipango miji na ramani za upimaji 16 zenye viwanja 3,104.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji huu umefanyika katika eneo lenye ukubwa wa ekari 1,892. Kamati ilifahamishwa kuwa, halmashauri imeanza awamu ya kwanza ya kuuzwa viwanja 1,248 kupitia mfumo wa TAUSI, viwanja 1,215 vimeshapandishwa katika mfumo kwa ajili ya kuuzwa na viwanja 33 vitamilikishwa kwa halmashauri kwa ajili ya huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, Hadi Kamati inautembelea Mradi huu, **Shilingi 1,040,288,619** zilikuwa zimekusanywa kutokana na uuzaji wa viwanja.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwepo kwa deni la **Shilingi 240,000,000** ambazo ni fedha za mkopo zilizotakiwa kurejeshwa baada ya Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi katika Mji wa

Mombo kukamilika. Kamati inaitaka Halmashauri kurejesha fedha hizo ambazo ni *revolving fund* ili halmashauri nyingine zinufaike. Vilevile, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuwa, shughuli zote zilizobaki katika kukamilisha mradi huu, zinafanyika chini ya usimamizi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Aidha, uwekwe utaratibu utakaowawezesha wananchi wenyeji wa eneo hili kupewa kipaumbele wakati wa upimaji na umilikishaji ili wapate ardhi katika mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Kupitia mradi huu kamati inaliona lengo zuri la serikali kuondoa/kupunguza migogoro ya ardhi, kuboresha miji na kuongeza mapato. Hata hivyo, ni vizuri Serikali ihakikishe zoezi hili linawanufaisha walengwa katika maeneo yote ambayo Miradi hii inatekelezwa. Kwa maeneo ambayo wananchi hawana uelewa wa mfumo unaotumika kununua na kuuza viwanja, wawekewe utaratibu maalum wa kusaidiwa ili kutoibua migogoro mingine.

(c) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Makazi na Biashara la Mkwakwani Commercial Complex chini ya NHC

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Mkwakwani Plaza wa Ghorofa 7 unatekelezwa kwenye Kiwanja Na. 55 A & B, Mtaa wa Mkwakwani

katika Jiji la Tanga. Jengo hili limekusudiwa kutumika kwa ajili ya shughuli za biashara, ofisi na nyumba za makazi.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu utagharimu **Shilingi 8,656,365,525.18** na unatarajiwa kutekelezwa kwa muda wa miezi 24 kuanzia tarehe 18 Juni, 2025 hadi 17 Juni, 2027. Hadi Kamati inautembelea, tarehe 18 Machi, 2026, Mradi ulikuwa umetumia **Shilingi 1,806,630,734.16** na ujenzi ulikuwa umefikia asilimia 36.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliridhishwa na malengo pamoja na hatua za utekelezaji wa Mradi huu na kuitaka Serikali kuhakikisha unakamilika kwa wakati na kwa kuzingatia thamani ya fedha. Aidha, Kamati inashauri Shirika la Nyumba kutekeleza yafuatayo: -

- (i) kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kukarabati majengo yake yaliyochakaa; na
- (ii) kuweka mipango ya kujenga nyumba za gharama nafuu ili kuboresha maisha ya wananchi wa kipato cha chini.

2.2.2.2 Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03)

Mradi Na. 4951: Upangaji wa Matumizi ya Ardhi, Halmashauri ya Mji wa Muheza

Mheshimiwa Spika, Mradi huu ulitengewa **Shilingi 124,768,000** na ulihusisha vijiji nane (8) vya Mindu, Lunguza, Mkuzi, Mgome, Mpapayu, Ubembe, Misongeni na Enzi ambapo kila kijiji kilitengewa **Shilingi 15,596,000**. Lengo la Mradi huu ni kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliutembelea Mradi huu tarehe 17 Machi, 2026 na imeridhishwa na kasi ya utekelezaji. Pamoja na hayo, Kamati inashauri yafuatayo: -

- (i) Wananchi waendeleo kupatiwa elimu juu ya thamani ya ardhi baada ya upimaji na umuhimu wa kuitunza na kuiendeleza;
- (ii) Serikali iongeze kasi ya kupeleka Miradi hii kwenye vijiji vingine hapa nchini ili kutatua migogoro; na
- (iii) Serikali iongeze kasi ya kutoa hati za kimila kwenye maeneo yaliyopimwa ili kukamilisha umiliki.

2.2.2.3 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi

Mheshimiwa Spika, Katika ziara za ukaguzi wa Miradi inayotekelezwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na

Maendeleo ya Makazi, Kamati ilipokea Taarifa za Utekelezaji wa Miradi na kuona hali halisi ya utekelezaji wa Miradi husika. Lengo likiwa ni kulinganisha na kubaini iwapo taarifa zilizowasilishwa na Wizara zinawiana na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji pamoja na madhumuni ya Miradi inayohusika. Tathmini ya kina imebainisha yafuatayo: -

- (i) Baadhi ya halmashauri kutorejsha fedha za mkopo za Mradi wa KKK kwa wakati na wengine kuzitumia kwa matumizi tofauti na hivyo kuzinyima halmashauri zingine fursa ya kupata mkopo huo;
- (ii) Wananchi wengi hasa wa maeneo ya vijijini hawana elimu juu ya matumizi ya mfumo wa e.Ardhi pamoja na TAUSI na hivyo kukosa fursa zinazopatikana kwenye mifumo hiyo;
- (iii) Kukosekana kwa miundombinu muhimu kama barabara, maji na umeme kwenye baadhi ya Maeneo ya Mradi wa KKK kunapunguza hamasa na kasi ya wananchi walionunua maeneo kuyaendeleza; na
- (iv) Baadhi ya wananchi kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya Mradi wa Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa na hivyo kuleta ugumu kwa baadhi ya maeneo.

2.2.3 Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

Mheshimiwa Spika, Lengo la uchambuzi wa taarifa za makusanyo ya maduhuli ni kuliwezesha Bunge kubaini iwapo makisio ya makusanyo yaliyoidhinishwa na Bunge yamefikiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Fungu 48 lilikadiriwa kukusanya **Shilingi 290,000,000,000** na Fungu 03 lilikadiriwa kukusanya **Shilingi 1,018,000,000**. Hadi kufikia mwezi Mei, 2026 Wizara ya Ardhi (Fungu 48) ilikuwa imekusanya **Shilingi 191,900,000,000** sawa na **asilimia 66.17**. Aidha, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) ilikuwa imekusanya **Shilingi 243,354,000** sawa na **asilimia 24** ya lengo. Taswira ya ukusanyaji inaonekana kwenye Kielelezo Na. 1.

Kielezo Na. 1: Ukusanyaji wa Maduhuli kufikia Mei, 2026

Fungu	Makadirio	Makusanyo	Asilimia
Wizara (48)	290,000,000,000	191,900,000,000	66.17
Tume (03)	1,018,000,000	243,354,000	24

Chanzo: Randama za Wizara 2026 na usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo:-

- (i) Ukusanyaji wa maduhuli kwa upande wa Wizara - Fungu 48 umefikia **asilimia 66.17** ya lengo. Kwa

kuangalia muda uliotumika na makusanyo, Kamati haioni ni kwa namna gani Wizara inaweza kufikia lengo la makusanyo; na

- (ii) Tume - Fungu 03 hadi Kamati inafanya uchambuzi, makusanyo yalikuwa **asilimia 24**. Kamati inaona ni vigumu kufikia lengo kwa mwenendo huu wa makusanyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha inaimarisha mikakati yake ya kukusanya maduhuli na pia kuziba mianya ya upotevu wa makusanyo.

2.2.4 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi - **Fungu 48** iliidhinishiwa **Shilingi 217,574,892,670**, ambapo **Shilingi 91,380,038,000** ni fedha za matumizi ya kawaida na **Shilingi 126,194,854,670** ni fedha za miradi ya maendeleo. Aidha, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (**Fungu 03**) iliidhinishiwa **Shilingi 12,708,185,000**, ambapo **Shilingi 8,187,569,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 4,520,616,000** ni fedha za maendeleo. Kamati ilipokea na kuchambua mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kama ifuatavyo:-

(a) **Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Februari, 2026, **Fungu 48** - Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 124,999,874,345.18**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 34,687,284,658.48** sawa na asilimia 64.45 ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 24,675,564,016.64** sawa na asilimia 65.69 matumizi mengineyo na **Shilingi 65,637,025,670** sawa na asilimia 94 fedha za ndani za maendeleo. Aidha, fedha za nje za maendeleo hazikupatikana. Mwenendo wa upatikanaji wa fedha ni kama unavyoonekana katika Kielelezo Na. 2.

Kielezo Na. 2: Upatikanaji wa Fedha kwa Fungu 48

MATUMIZI	KIASI KILICHOIDHINISHWA	KIASI KILICHOPOKELEWA	ASILIMIA
MISHAHARA (OC)	53,820,915,000	34,687,284,658.48	64.46
	37,559,123,000	24,675,564,016.64	65.68
JUMLA	91,380,038,000	59,362,848,675.12	64.96
MAENDELEO NDANI	69,869,494,670	65,637,025,670	94.00
MAENDELEO NJE	56,325,360,000	0	0
JUMLA	126,194,854,670	65,637,025,670	52
JUMLA KUU	217,574,892,670	124,999,874,345	57.44

Chanzo: Randama ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umeonesha yafuatayo: -

- (i) Hali ya upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo unaridhisha isipokuwa upatikanaji wa fedha za nje za Miradi hauridhishi; na
- (ii) Kukosekana kwa fedha za nje kunaweza kusababisha Miradi kuathirika na kuongezeka kwa muda wa utekelezaji unaoweza kuambatana na nyongeza ya gharama.
- (b) **Fungu 03 - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2026, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi - **Fungu 03**, ilikuwa imepokea **Shilingi 9,023,839,791.68** sawa na asilimia asilimia 71. Kati ya fedha hizo **Shilingi 2,826,395,000** sawa na asilimia 60 ni fedha za mishahara, **Shilingi 1,676,828,791** sawa na asilimia 48.24 fedha za matumizi mengineyo na **Shilingi 4,520,616,000** sawa na asilimia 100 ni fedha za miradi ya maendeleo. Kielelezo Na. 3 kinaonesha mwenendo wa upatikanaji wa fedha.

Kielezo Na. 3: Upatikanaji wa Fedha (Fungu 03)

UPATIKANAJI WA FEDHA FUNGU 03 MWAKA 2025/2026			
MATUMIZI	KILICHOIDHINISHWA	KILICHOPOKELEWA	%
MISHAHARA	4,712,143,000	2,826,395,000	60
(OC)	3,475,426,000	1,676,828,791.68	48.24
JUMLA	8,185,569,000	4,503,223,791	53.4
MAENDELEO (NDANI)	4,520,616,000	4,520,616,000	100
JUMLA	4,520,616,000	4,520,616,000	100
JUMLA KUU	12,708,185,000	9,023,839,791.68	71

Chanzo: Randama ya Wizara na usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo: -

- (i) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha wa asilimia 71 kwa ujumla unaridhisha;
- (ii) Upatikanaji wa asilimia 48.24 ya fedha za matumizi mengineyo hauridhishi na unaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli za Tume; na
- (iii) Upatikanaji wa asilimia 100 ya fedha za maendeleo unaonesha kuwa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa na Tume kwa mwaka wa fedha 2025/2026 unaweza kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hali ya upatikanaji wa bajeti ya Tume kuonesha mwelekeo mzuri, bado kiwango kinachotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo hakiridhishi katika kufikia lengo la kupanga matumizi ya ardhi kwa kila kipande cha ardhi nchini. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kupanga matumizi ya ardhi yote Tanzania ili kuepuka migogoro ya ardhi.

2.3 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua na kujadili Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

- (i) Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027;
- (ii) Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027;
- (iii) Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa; na
- (iv) Mambo mahususi yanayogusa Sekta ya Ardhi.

2.3.1 Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

(a) Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka Fedha 2026/2027 Wizara inakadiriwa kukusanya **Shilingi 300,000,000,000**. Kamati ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana katika ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Taswira ya ulinganisho wa makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na 2026/2027 inaonekana katika Kielelezo Na. 4.

Kielezo Na. 4: Ulinganisho wa Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027 Fungu 48

ULINGANISHO WA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2025/2026 NA 2026/2027 (FUNGU 48)				
CHANZO	2025/2026	2026/2027	Nyongeza/ Pungufu%	Nyongeza/ Pungufu%
	290,000,000,000	300,000,000,000	10,000,000,000	3

Chanzo: *Randama ya Wizara na usanifu wa Kamati*

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi unaonesha kuwa: -

- (i) Makadirio ya makusanyo yameongezeka kwa asilimia 3 ukilinganisha na mwaka unaoisha; na

- (ii) Kwa kuzingatia hali ya makusanyo ya asilimia 66.17 na muda wa miezi 11 uliotumika, Kamati ina mashaka ikiwa nyongeza ya asilimia 3 ya makadirio inaweza kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuweka na kusimamia mikakati ya ukusanyaji wa maduhuli yake ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

(b) Fungu 03 – Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Tume inakadiriwa kukusanya maduhuli ya **Shilingi 518,000,000** ambapo maduhuli yatokanayo na kodi ya pango yamelingana na makadirio ya mwaka unaoisha na maduhuli yatokanayo na michango ya wadau yamepungua kwa asilimia 50. Kielelezo Na. 5 kinafafanua.

Kielezo Na. 5: Ulinganisho wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2025/2026 na 2026/2027

ULINGANISHO WA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2025/2026 NA 2026/2027				
CHANZO	2025/2026	2026/2027	Nyongeza/ Pungufu	Nyongeza/ Pungufu%
Kodi ya Pango	18,000,000	18,000,000	-	-
Michango ya Wadau	1,000,000,000	500,000,000	(500,000,000)	50

Chanzo: Randama ya Wizara na usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo: -

- (i) Makadirio ya makusanyo kwa upande wa kodi ya pango yamelingana na makadirio ya mwaka unaoisha. Makusanyo ya maduhuli kwa mwaka unaoisha yalikuwa asilimia 35. Kamati haioni ni kwa namna gani makusanyo hayo yatafikia lengo ikiwa vyanzo na mikakati ya makusanyo ni ile ile; na
- (ii) Makadirio ya makusanyo kwa upande wa Michango ya Wadau yamepungua kwa asilimia 50. Hali hii inaakisi hali halisi ya makusanyo yaliyofikiwa ya asilimia 24 kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Kamati inaishauri Serikali kuongeza vyanzo vya mapato ambavyo ni vya uhakika ili kuhakikisha mapato hayashuki na lengo linafikiwa.

2.3.2 Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

(a) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza mpango na vipaumbele vilivyowekwa katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi - **Fungu 48** inaomba kutengewa **Shilingi 162,149,255,000** kulinganisha na Makadirio ya Matumizi ya **Shilingi 153,437,867,000** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Kwa kuzingatia takwa la Kanuni ya 120(2), Kamati imechambua Makadirio ya Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2026/2027 kwa kulinganisha makadirio hayo na Mwaka wa Fedha 2025/2026. Taswira hiyo inaonekana katika Kielelezo Na. 6.

Kielelezo Na. 6: Ulinganisho wa Bajeti ya Fungu 48 kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026 na 2026/2027

Na.	Maelezo		Kiasi cha fedha 2025/2026	Kiasi cha fedha 2026/2027	Ongezeko/pungufu	%
1.	Matumizi ya Kawaida	Mishahara	53,820,915,000	56,711,082,000	2,890,167,000	5.4
		Matumizi Mengineyo	37,559,123,000	33,803,211,000	(3,755,912,000)	10
	Jumla ndogo		91,380,038,000	90,514,293,000	(865,745,000)	1
2.	Matumizi ya Maendeleo	Fedha za ndani	5,732,469,000	5,732,469,000	0	0
		Fedha za nje	56,325,360,000	65,902,493,000	9,577,133,000	17
Jumla ndogo		62,057,829,000	71,634,962,000	9,577,133,000	15	
Jumla Kuu		153,437,867,000	162,149,255,000	8,711,388,000	5.7	

Chanzo: Randama ya Wizara na usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa: -

- (i) Bajeti ya mishahara imeongezeka kwa asilimia 5.4; na
- (ii) Bajeti ya Maendeleo imeongezeka kwa asilimia 15.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la bajeti ya maendeleo kwa asilimia 15 linaweza kuleta tija ikiwa fedha hizo zitapatikana kwa uwiano sahihi na kwa wakati.

(b) Fungu 03 – Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 48,110,260,000** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kulinganisha na Makadirio ya Matumizi ya **Shilingi 16,451,351,000** Mwaka wa Fedha 2025/2026. (Kielelezo Namba 7).

Kielezo Na. 7: Ulinganisho wa Bajeti ya Fungu 03 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027

Na.	Maelezo		Kiasi cha fedha 2025/2026	Kiasi cha fedha 2026/2027	Ongezeko/ pungufu	%
1.	Matumizi ya Kawaida	Mishahara	4,712,143,000	4,423,468,000	(288,675,000)	10
		Matumizi Mengineyo	3,475,426,000	3,127,883,000	(347,543,000)	10.6
	Jumla ndogo		8,187,569,000	7,551,351,000	636,218,000	8
2.	Matumizi ya Maendeleo		4,520,616,000	38,400,000,000	33,879,384,000	749.44
Jumla ndogo			4,520,616,000	38,400,000,000	33,879,384,000	749.44
Jumla Kuu			12,708,185,000	45,951,351,000	33,243,166,000	262

Chanzo: *Randama ya Wizara na usanifu wa Kamati*

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Bajeti ya Maendeleo imeongezeka kwa asilimia 749.44. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza Bajeti ya Maendeleo ambayo itakuwa na tija endapo itatoka kwa wakati na kuwezesha kupanga vijiji 1,492 kwa mwaka. Hii ina maana kwamba, kiwango hiki cha bajeti kikiendelea kutolewa, kazi ya upangaji wa vijiji 7,460 vilivyobakia nchini, itakamilika ndani ya miaka mitano.

2.3.3 Mambo Mahsusni Yanayogusa Sekta ya Ardhi

(i) Ukusanyaji wa Maduhuli

Mheshimiwa Spika, ardhi ni rasilimali muhimu ambayo ikisimamiwa vizuri inaweza kutoa mchango mkubwa kwenye pato la Serikali. Mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli ya Wizara hii kwa ujumla hauridhishi. Jambo hili linapunguza uchangiaji mapato ya ardhi katika pato la Taifa. Kamati inaishauri Wizara kuimarisha vyanzo na

ukusanyaji wa mapato kwa kuhakikisha taarifa za ardhi za kila mmiliki zinaingia kwenye mfumo rasmi wa malipo ili kurahisisha ufuatiliaji. Vilevile, Serikali ihakikishe wamiliki wote wa ardhi waliosajiliwa wanaingizwa kwenye mfumo wa kupata jumbe fupi za kukumbushia kulipa kodi kama ilivyo kwenye taasisi zingine mfano Mamlaka za Maji. Mfumo wa e.Ardhi pamoja na mifumo mingine irahisishwe ili wananchi wa kawaida wanufaike nayo.

(ii) **Migogoro ya Ardhi nchini**

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali za kutatua migogoro ya ardhi maeneo mbalimbali nchini, bado changamoto hii ni kubwa. Kamati imebaini kwamba, sababu za migogoro hii ni pamoja kuongezeka kwa ushindani wa matumizi ya Ardhi kunakosababishwa na ongezeko la watu sambamba na ongezeko la shughuli za kibinadamu, ukosefu na au kutokuzingatiwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi, kutokuwa na mfumo wa kidigitali wa usimamizi wa ardhi katika maeneo yote nchini hali inayorahisisha ardhi kumilikishwa mara mbilimbili (*Double Allocation*), kukosekana kwa usimamizi madhubuti wa sheria na baadhi ya watumishi wa ardhi kutokuwa waaminifu katika utekelezaji wa majukumu yao. Hali hii isipopatiwa ufumbuzi, migogoro itaendelea kuongezeka na kuathiri ustawi wa maisha ya kila siku ya wananchi. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi katika

upimaji, umilikishaji na usajili wa ardhi, uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi, usimamiaji sheria, ujenzi na usambazaji wa mfumo wa kidijitali wa kusimamia ardhi Nchini ili kuondoa migogoro pamoja na kuongeza pato la Taifa litokanalo na rasilimali ardhi.

(iii) **Kupanga, Kupima na Kumilikisha (KKK)**

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa mkopo wa **Shilingi Bilioni 50** kwa Halmashauri 57, Vyuho vya Ardhi vya Tabora, Morogoro, Chuo Kikuu cha Ardhi na Ofisi ya Ardhi kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha. Lengo likiwa ni kuziwezesha halmashauri hizo Kupanga na Kupima na Kumilikisha ardhi kwa kutumia fedha hizi (*revolving fund*) na kuzirejesha ili halmashauri zingine zinufaike. Hadi Kamati inakutana na Wizara, **Shilingi Bilioni 33.18** sawa na asilimia 66.4 zilikuwa zimerejeshwa. Taarifa zinaonesha kuwa, zipo Halmashauri ambazo zimekusanya fedha hizi na kuzitumia kwa matumizi mengine. Kwa kuwa fedha hizi ni za mzunguko (*Revolving Fund*), Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha Halmashauri zote ambazo hazijarejesha, zinarejesha ili kuziwezesha halmashauri zingine kutumia fedha hizo kwenye programu hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuweka mfumo maalumu wa kufuatilia na kuhakikisha fedha hizo

zinarejeshwa kwa wakati na kwenda moja kwa moja Wizarani na za Halmashauri ziende Halmashauri. Vilevile, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa, maeneo yote yanayopimwa yanawekewa miundombinu muhimu ili kurahisisha shughuli za kuendeleza maeneo hayo.

(iv) **Ubakishaji wa Asilimia 20 ya Makusanyo ya Kodi ya Pango la Ardhi (*Retention*)**

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fedha ya Mwaka 2024 ilifanya mabadiliko katika Sheria ya Serikali za Mitaa Sura 289 kuruhusu Halmashauri kubakisha asilimia 20 ya makusanyo ya kodi ya pango la ardhi kwa lengo la kuongeza kasi ya ukusanyaji wa kodi hiyo. Hata hivyo, kwa mujibu wa Kifungu cha 10 cha Sheria ya Ardhi Sura 113, jukumu la ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi ni miongoni mwa majukumu ya msingi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, ulipaji wa pango la ardhi ni miongoni mwa masharti ya msingi ya umiliki wa ardhi nchini na kutokulipwa kwa pango la ardhi ni moja ya sababu inayoweza kupelekea ubatilishwaji wa hati miliki, jambo linalopaswa kuratibiwa na kusimamiwa na Wizara ya ardhi. Licha ya mabadiliko hayo ya sheria ya mwaka 2024 kuelekeza asilimia 20 ya makusanyo ya Kodi kubaki

Halmashauri, serikali haijawahi kupeleka fedha hizo pamoja na mambo mengine sababu mojawapo ikiwa jukumu hilo kutokutekelezwa na halmashauri. Aidha, Wizara ndio inayomiliki na kusimamia kumbukumbu zote za wamiliki wa hati za Ardhi nchini. Ili kutekeleza jukumu la ukusanyaji pango la ardhi, wizara inalazimika kutumia fedha zake za ndani kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) kwa shughuli za ukusanyaji wa pango la ardhi.

Mheshimiwa Spika, Wizara kukosa fedha hizo inapunguza kasi ya ukusanyaji wa kodi pamoja na ujenzi wa mifumo ya kielektroniki ya utoaji wa huduma za ardhi (*e-Ardhi*). Ili kuimarisha mifumo ya taarifa za ardhi nchini, Serikali italazimika Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi nchi nzima; kuongeza na kutunza taarifa za walipa kodi; kuwatambua wamiliki wa ardhi; na kupunguza migogoro ya ardhi. Utekelezaji wa haya yote unahitaji bajeti ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kufanya mabadiliko katika Sheria ya Fedha na kuruhusu Wizara ya Ardhi kubaki au kurejeshewa asilimia 20 ya makusanyo ya kodi ya pango la ardhi ili fedha hizo zitumike kukamilisha shughuli tajwa kwa lengo la kuongeza kasi ya ukusanyaji wa kodi pamoja na kuboresha utoaji wa huduma kwa Wizara.

(v) **Uvamizi wa Maeneo ya Wazi (Open Spaces)**

Mheshimiwa Spika, utengaji na usimamizi wa maeneo ya wazi nchini unaongozwa na Sheria ya Mipango Miji, Sura 355 (*Urban Planning Act, Cap 355*). Sheria hii inazipa Mamlaka za upangaji jukumu la kutenga, kupima, kutunza na kulinda maeneo ya wazi chini ya Usimamizi wa Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, maeneo yote ya wazi kama vile viwanja vya michezo, bustani na maeneo ya kupumzikia ni mali ya umma na hayapaswi kubadilishiwa matumizi bila idhini maalum ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa maeneo mengi ya wazi ni vigumu kuyatambua kutokana na uvamizi unaofanywa na wananchi kwa kushirikiana na watumishi wa Wizara ambao huuziana kinyemela na kubadili matumizi. Vilevile baadhi ya mitaa haijatangewa kabisa maeneo hayo. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya kurejesha maeneo yote ya wazi yaliyovamiwa na kuhakikisha kuwa inasimamia kikamilifu utengaji na utunzaji wa maeneo ya wazi nchini.

(vi) **Shirika la Nyumba la Taifa (National Housing Corporation - NHC)**

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ni Taasisi ya Serikali inayosimamia na kuendeleza Sekta ya Ujenzi, Miliki na Makazi nchini. Miradi mikubwa ya Shirika

hili inajumuisha miradi ya makazi, majengo ya kibiashara, huduma za upangishaji na uwekezaji wa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2025 -2030 imelielekeza Shirika la Nyumba kujikita katika kuongeza upatikanaji wa nyumba bora na za gharama nafuu hususan mijini na maeneo yenye ukuaji wa kasi wa idadi ya watu; kuendeleza miradi ya nyumba na majengo ya biashara katika mikoa inayokua kwa kasi; kukuza ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi (PPP); na kuboresha mipango miji na matumizi ya ardhi ili kusaidia maendeleo ya makazi yaliyo rasmi na yenye huduma za msingi.

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati inalishauri Shirika la NHC kukamilisha miradi yake yote ambayo imechukua muda mrefu kukamilika, kufanya ukarabati wa nyumba zake za zamani zilizochakaa ili kuongeza mapato, kukuza, kupendezesha miji, kuongeza ustawi wa jamii. Aidha, kuna uhitaji mkubwa wa nyumba za gharama nafuu unaotokana na ukuaji wa miji kuliko uwezo wa uzalishaji. Kamati inaishauri Serikali kuliwezesha Shirika kujenga nyumba za gharama nafuu kuwasaidia wananchi wa makundi ya kipato cha chini na kati.

(vii) **Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Adhi**

Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (*National Land Use Plan Commission – NLUPC*) ilianzishwa mwaka 1984 chini ya Sheria ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Sura ya 116 ya Sheria za Tanzania. Tume hii iliundwa kwa lengo la kuratibu na kusimamia upangaji bora wa matumizi ya ardhi nchini ili kuhakikisha ardhi inatumika kwa tija, uendelevu na kupunguza migogoro ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Tume inakabiliwa na changamoto za upungufu wa rasilimali fedha unaopelekea utekelezaji wa mipango kuchelewa, kuibuka kwa migongano kati ya wakulima, wafugaji, wawekezaji, hifadhi na makazi. Katika vijiji 12,333 nchini ni vijiji 4,873 ndio vilivyoandaliwa mipango ya matumizi bora ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, ili Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, ni muhimu Serikali kuimarisha upatikanaji wa rasilimali fedha; kuhakikisha kunakuwepo na ushirikiano wa taasisi; itolewe elimu kwa wananchi; na uwepo wa matumizi ya teknolojia bora na za kisasa katika usimamizi madhubuti wa utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Baada ya uchambuzi kuhusu Utekelezaji wa Bajeti pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, sasa naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

3.1 Maoni ya Jumla

- (i) Serikali iongeze kasi ya kutoa elimu kwa jamii hasa vijana kuhusu taratibu za kumiliki ardhi kihalali na umuhimu wake;
- (ii) Wizara ya Ardhi iendeele kufanya maboresho ya kimfumo ili kuondoa kero na changamoto zilizopo; na
- (iii) Wizara iongeze kasi ya kupima na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji vyote nchini ili kuondoa migogoro ya ardhi nchini.

3.2 Ushauri wa Kamati katika Maeneo Mahsusi kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

a. Ukusanyaji wa Maduhuli

Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

- (i) Kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato kwa kuhakikisha taarifa zote za umiliki wa ardhi zinaingizwa kwenye mfumo rasmi wa malipo ili kurahisisha ufuatiliaji;

- (ii) Ihakikishe wamiliki wote wa ardhi waliosajiliwa wanaingizwa kwenye mfumo wa kupata jumbe fupi za kukumbushia kulipa kodi kama ilivyo kwenye taasisi zingine mfano Mamlaka za Maji; na
- (iii) Mfumo wa kidijitali wa uuzaji wa viwanja unakuwa rahisi na rafiki ili wananchi waweze kunufaika na fursa zinazotokana na mfumo huo.

b. Migogoro ya Ardhi Nchini

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

- (i) iongeze kasi katika kuandaa na kuweka mipango ya matumizi bora ya ardhi ili vijiji vyote vifikiwe na mipango hii.
- (ii) iongeze kasi ya kupima, kupanga, kumilikisha na kusajili haki miliki za ardhi kwa kila kipande cha ardhi ili kuondoa migogoro lakini pia kuongeza pato la Taifa litokanalo na rasilimali ardhi;
- (iii) iongeze huduma ya kliniki za ardhi katika mikoa yote nchini; na
- (iv) iwachukulie hatua kali na stahiki watumishi wote wanaojihusisha na vitendo vilivyo kinyume na Sheria.

c. Kupanga, Kupima na Kumilikisha (KKK)

Kamati inaishauri kuwa, Serikali:-

- (i) kuhakikisha Halmashauri zote ambazo hazijarejesha fedha za Mradi wa KKK zinarejesha ili kuziwezesha halmashauri nyingine kutumia fedha hizo kwenye programu hiyo;
- (ii) iweke mfumo maalum wa kufuatilia na kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa kwa wakati; na
- (iii) Kuhakikisha kuwa maeneo yote yanayopimwa yanawekewa miundombinu muhimu ikiwemo barabara ili kuhamasisha wamiliki kuendeleza maeneo hayo.

d. Mfumo Unganishi wa Kielektroniki wa Huduma za Ardhi (e-Ardhi)

Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

- (i) ihakikishe inaongeza kasi ya kusambaza Mfumo wa *e-Ardhi* kwenye halmashauri zote nchini ili shughuli zote zinazohusiana na ardhi zifanyike kwenye mifumo; na
- (ii) ihakikishe inatoa elimu kwa wananchi na mafunzo endelevu kwa Maafisa Ardhi kuhusu Mfumo wa utoaji huduma katika usimamizi wa Ardhi.

e. Ubakishaji wa Asilimia 20 ya Makusanyo ya Kodi ya Pango la Ardhi (Retention)

Kamati inaishauri Serikali kufanya mabadiliko katika Sheria ya Fedha na kuruhusu Wizara ya ardhi kubaki na

asilimia 20 ya makusanyo ya kodi ya pango ili fedha hizo zitumike kuwezesha shughuli za ufuatiliaji na ukusanyaji kodi ya pango la ardhi sambamba na kusaidia ujenzi na usambazaji mfumo wa kidijitali wa usimamizi wa Ardhi nchini.

f. **Shirika la Nyumba la Taifa (National Housing Corporation - NHC)**

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

- (i) ijenge nyumba za gharama nafuu katika maeneo mbalimbali nchini ambazo wananchi wa kipato cha chini na kati wataweza kuzimudu;
- (ii) ianzishe mifumo rafiki ya TEHAMA katika usimamizi wa nyumba, upangishaji na uuzaji;
- (iii) ifanye uhakiki wa wapangaji halali walioko kwenye nyumba za Shirika;
- (iv) ikamilishe Miradi yake iliyochukua muda mrefu bila kukamlika; na
- (v) ichukue hatua za kisheria kwa wadaiwa sugu.

g. **Uvamizi wa Maeneo ya Wazi (Open Spaces)**

Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

- (i) Ifuatilie na kurejesha maeneo yote ya wazi yaliyovamiwa pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria wahusika; na

- (ii) Ihakikishe kuwa inasimamia kikamilifu utengaji na utunzaji wa maeneo ya wazi nchini.

h. Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Adhi

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

- (i) itoe elimu kwa wananchi kuhusu manufaa yanayopatikana kutokana na kazi ya uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi sambamba na usimamizi wa mipango hiyo;
- (ii) iongeze elimu kwa umma kuhusu faida za mipango ya matumizi ya ardhi;
- (iii) iendelee kutoa fedha ili kazi ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ikamilike kwa vijiji vyote nchini;
- (iv) ikamilishe hatua zote sita za uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi ili kufikia hatua ya mwisho ya utoaji wa hati miliki za kimila na kupunguza migogoro, kuongeza thamani ya ardhi na kuwafanya wananchi wanufaike na fursa mbalimbali zikiwemo zinazopatikana kwenye taasisi za fedha.

3.3 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru na kukupongeza kwa kuliongoza Bunge letu kwa umahiri. Vilevile, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Naibu Spika - Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb) na Wenyeviti wa Bunge, kwa kukusaidia kuongoza Vikao vya Bunge kwa umahiri.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa namna walivyojitoa wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha Maoni kuhusu Bajeti ya Wizara hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Orodha yao ni kama inavyoonekana hapa chini na kwa ruhusa yako, naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*):-

1. Mhe. Timotheo Paul Mnzava, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Mary Francis Masanja, Mb -M/Mwenyekiti
3. Mhe. Festo Richard Sanga, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Haidary Hemed Sumry, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Cosmas Mtesigwa Bulala, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Fadhili Fabian Ngajilo, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Silvery Luboja Salvatory, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Yannick Ikaya Ndoinyo, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Chiku Athman Issa, Mb - Mjumbe

10. Mhe. Rashid Mohamed Mtima, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Selina Henry Kingalame, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Mvita Mustafa Ali, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Khamis Ali Vuai, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Hadija Shabani Taya, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Joshua Samwel Nassari, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Asia Abdulkarim Halamga, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Issa Ally Mchungahela, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Amina Good Said, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Dkt. Leonard Douglas Akwilapo, Mb - Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. Kaspar Kaspar Mmuya, Mb - Naibu Waziri, Dkt. Anthony Sanga - Katibu Mkuu na Bi. Lucy D. Kabyemera – Naibu Katibu Mkuu pamoja na Watumishi wote wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa kuwa mstari wa mbele kutoa ushirikiano kwa Kamati muda wote walipohitajika.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Katibu wa Bunge - Ndg. Baraka I. Leonard, kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na kuhakikisha inatekeleza majukumu iliyopangiwa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.



Mhe. Timotheo Paul Mnzava, Mb

MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII

28 Mei, 2026